Sera zinarekebishwa mara kwa mara. Kwa toleo la hivi karibuni. Tafadhali tembelea tuvuti yetu https://salkeiz.sharepoint.com/qam/SitePages/Home.aspx

1. Wanafunzi wote, wanafanyakazi na wageni katika wilaya ya shule za Salem-Keizer wanahaki ya kusoma, kufanya kazi na kushiriki katika mazingira salama na huru kutoka ubaguzi, ukali, na kutishwa. Wilaya imejidhatiti kutoa mazingia salama na mazingira yanayo karibisha.

2. UFAFANUZI:

2.1. UHUISHAJI: Hali ya kusikia hasira au chuki kuelekea siku au mtu.

2.2. Tukio la Upendeleo: Usemi wa uadui wa mtu dhidi ya mtu mwingine, uhusiano wa mtu mwingine kuhusiana na rangi ya mtu, rangi ya utambulisho, dini,utambulisho wa jinsia, mwelekeo wa kijinsia, ulemavu au asili ya kitaifa, ambayo uchunguzi wa jinai au mashtaka haiwezekani au haifai. Tukio la upendeleo linaweza kujumuisha lugha ya kudhalilisha au tabia elekezi kwa au kuhusu kikundi chochote cha idadi ya watu waliotangulia.

2.3. Mtu Aliyeathirika: Mtu anayedaiwa kuwa ni muathirika wa mwenendo ambao unaweza kusababisha tukio la upendeleo. Hii inajumuisha mtu binafsi ambaye tukio limeelekezwa kwake moja kwa moja kama mwanafunzi au mfanyakazi katika jamii kundi kubwa ya shule inayoweza kuathiriwa na tukio hilo.

2.4. Nembo Ya Chuki: Nembo, picha au kitu ambacho huonyesha uhuishaji hali kuzingatia na rangi ya mtu, rangi ya utambulisho, dini,utambulisho wa jinsia, mwelekeo wa kijinsia, ulemavu au asili ya kitaifa, kujuisha kitanzi, nembo ya fikra za neo-Nazi na bendera ya vita kwenye ushirika na wanaonyesha:

- Kuna uwezakano wa kusababisha usumbufu mkubwa au kuingiliana na nyezo za shule pamoja na shughuli, au
- Kuna uwezakano wakuingiliana na haki haki za wanafunzi kwa kukataliwa kupata huduma, shughuli za shule na nafasi zinazotelewa na shule

.

3. MWENENDO MARUFUKU

3.1. Wilaya inakataza na kupiga marufuku matukio ya upendeleo kwenye mazingira ya wilaya za shule au kwenye programu za wilaya, huduma, shule au shughuli. Hii inajuimusha uso kwa uso, simu za mtandao, maonyesho ya dijiti au mwili kwenye mali ya binafasi.

3.2. Uwepo wa nembo ya chuki kulingana na na rangi ya mtu, rangi ya utambulisho, dini,utambulisho wa jinsia, mwelekeo wa kijinsia, ulemavu au asili ya kitaifa, nyezo na usumbufua mkubwa katika shughuli za shule na mazingira ya kujifunzia na mazingira ya kazi na kuunda mazingira ya hofu na vitisho na woga na kuingiliana na haki za mwanafunzi na wafanyakazi kwa kukataa kutoa huduma zote, shughuli au fursa zinazotelewa na shule au idara. Utumiaji au kuonyesha nembo ya chuki kwenye mazingira ya wilaya ya shule au kwenye programu, huduma, shule na shughuli ni marufuku kabisa. Hii inajumuisha uso kwa uso, simu za mtandao, maonyesho ya dijiti au mwili kwenye mali binafsi.

3.2.1. Isipokuwa pale tu hiyo nembo inaonyeshwa kama sehemu iliyorusiwa kama sehemu ya mtaala unaoendana na viwango vya Oregon State.

I

4. KUTOA TAARIFA NA KUJIBU

4.1. Taarifa zote kuhusu tukio la upendeleo litachunguzwa na kuelezea kufuata mwongozo ulioweka na Superintedent angalia ADM-P010

4.2. Wanafunzi, wazazi/walezi, wageni na jamii wanahamasishwa kutoa taarifa ya tukio la upendeleo na nembo ya chuki kwa wasimamazi wa shule/idara ya wasimamizi au kwa mfanyakazi wa wilaya ya shule.

4.3. Mfanyakazi atatakiwa kutoa taarifa ya tukio la upendeleo mara moja na kuonyeshwa kwa nembo ya chuki ambayo mfanyakazi ameona au imetolewa taarifa na mtu wa watatu, kwa wasimamazi wa shule/wasimamazi wa idara kuchukua hatua mara moja kuwakikisha usalama wa wanafunzi, wafanyakazi na wageni.

4.4. Mfanyakazi yeyote atakaye jibu taarifa ya tukio la upendeleo (kujumuisha wanafanyakazi wale waliopokea taarifa, mashahidi wa tukio la upendeleo au nembo ya chuki, au wanahusika na uchunguzi) watazingatia yafuatayo katika kujibu:

- Tambua uzoefu wa kila mtu aliyeathiwa;
- Tambua athari kwa mtu anayeripoti tukio la upendeleo
- Kujitolea kuchukua hatua mara moja na
- Kuzuia madhara zaidi dhidi ya watu waliothariwa kutokea

4.5. Wasimamizi wa shule/wasimamizi wa idara watahakikisha kuwa watu wote waliothirika na taarifa ya upendeleo wanapata taarifa. Taarifa itafuata na kutolewa kwa mtu ambaye tabia imelekezwa kwake, mtu aliyefanya tabia hiyo na wanafunzi katika jamii ya shule wanaoweza kuathiriwa na tukio hilo:

4.5.1. Taarifa_kuonyesha kuwa uchunguzi umeanza

4.5.2. Hatua zimechukuliwa kuzuia kurudia

Taarifa ifuatayo itatolewa kwa mtu ambaye tabia ili elekezwa na mtu aliyefanya hiyo tabia:

4.5.3 Taarifa kuonyesha kuwa uchunguzi umekamalika; na

4.5.4 Matokeo ya uchunguzi na uamuzi wa mwisho kutokana na yale matokeo

Kama itatokea kuwa taarifa kwenye sehemu 4.5.1 mpaka 4.5.4 haziwezi kushirikikisha kwa sababu yeyote, kujumuisha haki ya usiri Federal Educational Rights and Privacy Act (FERPA) au aina nyingine ya sheria ya usiri, wasimamizi wa shule/wasimamazi wa idara watatoa nukuu kwamba sheria inawazuia kutoa taarifa na kuelezea jinsi sheria inavyoelekeza.

4.6. Kama mtu atakutwa kavunja hii sera, wilaya inatachukua hatua inayofaa ya kurekebisha na kuangalia jinsi ya kumuelimisha muhusika kutokana na vitendo vyao na hatua za kurekebisha adhabu.

4.7. Mfanyakazi atakaye kiuka sera hii anaweza kuchukuliwa hatua za kinidhamu.

4.8. Wasimamizi wa shule/wasimamizi wa idara watapitia matokeo ya uchunguzi na baraza kwenye ngazi ya usimamazi wakati wakifikiria kuwa ikiwa hatua nyingine zinahitajika kuchukuliwa ili kuzingatia haki za kibinadamu. Baraza ngazi ya usimamazi wanaweza kushauriana na wilaya nyingine nje au rasimali za nje wakati wanafanya maamuzi.

4.9. Mtu anaweza kuomba wilaya ipitie hatua zilizochukuliwa na mfanyakazi katika kujibu na au uchunguzi wa taarifa kwa kujaza ombi la maandishi kwa Superintendent. Uhakiki unaweza kufanywa na msaidizi wa Superintendent au mtu aliyeteuliwa. Maombi lazima ya tumwe ndani ya siku 10 za kazi ya mtu anayepokea taarifa kwenye matokeo ya uchunguzi.

4.10. Mtu binafsi ana haki ya kukata rufaa maamuzi ya mwisho ya wilaya kwa idara ya elimu Oregon au idara ya elimu ya US ofisi ya haki za binadamu

5. ULINZI

5.1. Kuanza kwa malalamiko kwa nia njema juu ya tabia ambayo inaweza kukiuka sera hii inaweza isiathiri vibaya:

- Majukumu ya kielimu au mazingira ya kielimu ya mwanafunzi au mtu mwingine aliyeanzisha malalamiko, kutoa ripoti ya tabia hiyo, au kushiriki katika uchunguzi; na
- Mkataba au hali ya ajira au kazi au mazingira ya elimu ya mfanyakazi wa wilaya au mtu mwingine anayeanza malamiko, kutoa ripoti ya tabia, au kushiriki kwenye uchunguzi

5.2. Juhudi zitafanywa kutoa unafuu unaofaa kwa watu waliothiriwa, pamoja na kuzuia na au kuchukua hatua za marekebisho zidi ya kulipiza kisasi. Kulipiza kisasi dhidi ya watu wanoanzisha malalamiko au vinginevyo wanaripoti matukio yaliyofunikwa na sera hii au wale wanaoshiriki kwenye uchunguzi au shughuli zingine zinazohusiana ni marufuku. Mtu yeyote anayepata kisasi anahimizwa kutoa ripoti kwa msimamizi wa shule au idara ya wasimamizi. Wafanyakazi pia wanaweza kutoa ripoti kuhusu visasi kwa afisa mwajiri wa wilaya/mwajiri na mahusiano. Mwanafunzi na wazazi/walezi pia wanaweza kutoa ripoti ya kisasi kwa wilaya kwenye ofisi ya elimu kwa k-12

6. MATANGAZO:

6.1. Hii sera itakuwa:

- Itachapishwa kwenye mtandao wa wilaya ya shule website;
- Itakuwa inapatikana kwenye shule zote za wilaya 24J ofisi za shule na ofisi za wilaya Itatolewa kwa ombi kwa wanafunzi, wazazi/walezi, wafanyakazi wa wilaya na wageni; na
- Nakala ya hii sera walau ukubwa wa 8.5" x 11 itabandikwa kwenye shule za sekondari na high

7. MAFUNZO:

7.1. Wasimamizi wa wilaya wataunda na kutekeleza vifaa vya kufundishia ili kutengeneza sera hii na mazoea yanayohusiana ikiwa ni pamoja na taratibu za kuripoti, mchakato wa elimu na athari zinazojulikana kwa wafanyakazi wote na wanafunzi.

Kutekeleza Taratibu na Sera Zinazoambatana:

ADM-P010 "Kuchunguza taarifa ya tukio la upendelo na nembo ya chuki"

INS-A003 "Kuhangaisha, Unyanyasaji, Vitisho, Uonevu, Mwanafunzi anayetisha na uonevu wa kimtandao"

HUM-A029 "Unyanyasaji wa kijinsia"

HUM-A018 "Unyanyasaji sehemu ya kazi"

Revision History:

Date	Description
11/23/20	New policy
4/12/21	Updated 2.4 (examples of symbols of hate) and 4.5 (notifications)

Approved By:_____ **Assistant Superintendent**